

Mabadiliko ya Damu ya Mwezi zako ni **KAWAIDA** wakati unapotumia Njia za Kupanga Uzazi

Ni kawaida kuwa na mabadiliko ya damu ya mwezi wakati unapotumia njia za Kupanga Uzazi.*


Angalia upya fomu hii ya kufanya kazi kama Moja ya vifaa vya ushauri wakati unapochagua njia ya Kupanga Uzazi.



*Mabadiliko ya kawaida katika damu ya mwezi ni kama vile Hedhi nyepesi (damu inayotoka kidogo tu), Hedhi za mda mfupi, Hedhi nzito (damu inayatoka sana), Hedhi za mda mrefu, Hedhi wakati hizitarajii, ama Hedhi kuacha kutoka kwa muda (kwa mfano, unapotumia njia za Kupanga Uzazi damu itaacha kutoka kwa muda au kabisa wakati unatumia njia hiyo).

Zungumza na Daktari wako kama uko na maswali yoyote ama wasiwasi wakati wowote.

N Ni **KAWAIDA** na salama kuwa na mabadiliko katika Hedhi (damu ya mwezi) wakati unapotumia njia za Kupanga Uzazi.*



O Hedhi (damu ya mwezi) inayotoka kidogo, ama Hedhi kuacha kutoka kwa muda* inaweza kutoa **NAFASI** kwa kukupa nguvu na uhuru kuendelea na shughuli zako.



R Damu ya mwezi yako na uzazi **ITARUDI** unapoacha matumizi ya njia za Kupanga Uzazi.



M **NJIA** tofautitofauti za Kupanga Uzazi zinaweza kusababisha mabadiliko katika damu ya mwezi. Zungumza na Daktari wako kuhusu mahitaji yako.



A **KUKOSEKANA** kwa damu ya mwezi haimanishi kwamba umepata mimba.




L Zungumza na Daktari wako kama mabadiliko katika damu ya mwezi **HUZUIA** shughuli zako. Labda kunaweza kuwa na tiba zinazoweza kusaidia.




Njia tofautitofauti za Kupanga Uzazi zinaweza kusababisha mabadiliko tofautitofauti ya Hedhi

Hapa chini kuna baadhi ya mabadiliko ya Hedhi ya kawaida, **lakini kila mmoja ni tofauti**. Labda unaweza kuhisi mabadiliko haya, baadhi yao, ama yote.



SINDANO ya Kupanga Uzazi

- Kupata Hedhi wakati usipotarajia
- Madoa ama tone ya Hedhi
- Damu ya mwezi nyepesi (kidogo tu)
- Hedhi nzito
- Hedhi kuacha kutoka kwa muda



VIPANDIKIZI vya Kupanga Uzazi

- Kupata Hedhi wakati usipotarajia
- Madoa ama tone ya Hedhi
- Damu ya mwezi nyepesi (kidogo tu)
- Hedhi nzito
- Hedhi kuacha kutoka kwa muda



VIDONGE (Vya homoni ya Progestin pekee)

- Hedhi ya mda mfupi
- Damu ya mwezi nyepesi (kidogo tu)
- Madoa ama tone ya Hedhi
- Hedhi kuacha unaponyonyesha
- Kupata Hedhi wakati usipotarajia
- Hedhi ya mda mrefu




VIDONGE (Vyenye mchanganyiko wa Homoni)

- Hedhi ya mda mfupi
- Damu ya mwezi nyepesi (kidogo tu)
- Madoa ama tone ya Hedhi



KITANZI cha IUD

- Hedhi ya kawaida
- Hedhi nzito
- Hedhi ya mda mrefu



HOMONI za IUD

- Kupata Hedhi wakati usipotarajia
- Madoa ama tone ya Hedhi
- Damu ya mwezi nyepesi (kidogo tu)
- Hedhi isiyotoka mara kwa mara
- Hedhi kuacha kutoka kwa muda

KUMBUKA: Kuwa damu yako ya mwezi ikiacha kutoka kwa muda wakati unatumia njia za Kupanga Uzazi, ni **KAWAIDA**. Kunaweza kuwa hata na faida kwa afya au maisha yako.

Zungumza na Daktari wako kama uko na maswali yoyote ama wasiwasi wakati wowote.